**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

**SHULE YA SEKONDARI BWIRU GIRLS'**
**S.L.P 170**
**MWANZA**

**Kumb. Na.BG/SS/JI/F5/36** **...../..../2026**

**Namba za Simu**
**MKUU WA SHULE; 0743350734**
**M/ MKUU WA SHULE; 0678100559**
**M/ MALEZI: 0768878689**
**M/TAALUMA: 0755922222**

Jina la mwanafunzi**.....................................................................**

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BWIRU GIRLS' ILIYOPO MANISPAA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA KWA KIDATO CHA TANO MWAKA 2026/2027.**

**1.0. UTANGULIZI**.

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato cha tano (5)** katika shule hii **mwaka 2026/2027.** Shule ya sekondari ya BWIRU GIRLS' iliyopo mkoani **Mwanza** Manispaa ya ILEMELA Kata ya Pansiasi. Shule inafikika kiurahisi kwani kuna usafiri wa magari ya abiria (daladala) kutoka mjini hadi Bwiru. Magari hayo yanapatikana kwenye stendi ya Bwiru iliyopo karibu na soko la makoroboi Mwanza mjini.

Mwaka wa masomo utaanza **TAREHE 01/7/2026 hivyo** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **TAREHE 29/6/2026** kabla ya saa 10:00 jioni tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.

# MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

## A: SARE YA SHULE

(a) Sketi mbili (2) ndefu **usawa wa katikati ya goti na enka** za rangi **NYEKUNDU kitambaa cha suti namba 1** zenye rinda box mbele na nyuma na marinda matatu kila upande mbele na nyuma kwa matumizi ya darasani. Inapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 25,000/= kila moja (Muislam atashona ndefu hadi kwenye enka na Hijabu,pia inaweza kupatikana shuleni kwa bei ya Tsh, 35,000/=) kwa atakayependa kushonea shuleni

(b) Gauni mbili ndefu usawa wa enka za rangi ya **blue Bahari (light blue) kitambaa cha kreta** namba 1 mshono wa solo yenye mikanda inayofungwa nyuma kwa matumizi baada ya vipindi. Linapatikana shuleni kwa bei ya Tsh, 45,000/= kila moja kwa atakayependa kushonea shuleni

(c) Shati mbili zenye mikono mirefu za rangi **nyeupe kitambaa cha halua** zisizo na urembo za kufungwa kwa vishikizo vya kawaida zilizodaliziwa nembo ya shule (inapatikana shuleni kwa bei ya Tsh, 20,000/= kila moja kwa atakayependa)

(d) Fulana 2 za rangi ya **blue bahari** zenye ukosi **mweusi** wenye michirizi ya blue bahari zisizo na maandishi bali ziwe na nembo ya shule mbele na maandishi ya moto wa shule kwa nyuma (kwa matumizi baada ya vipindi vya darasani).inapatikana shuleni kwa bei ya Tsh, 15,000/= kwa kila moja kwa atakayependa kununulia shuleni.
(e) Viatu **vyeusi** jozi mbili(2) vya Ngozi laini ya mng'ao visivyotumia rangi na visivyo na kisigino wala mfano wa buti(simple) visivyo na urembo.
(f) Soksi nyeupe ndefu hadi magotini zisizo na urembo (stocking) bali ziwe na michirizi ya rangi nyekundu zenye jina la shule (zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 4000=@) jozi2
(g) Sweta 1 rangi nyeusi **lenye nembo ya shule. Linapatikana kwa Tsh. 15,000/=**
(h) Tai mbili (2) za rangi ya rangi **nyekundu yenye michirizi ya nyeupe** zenye nembo ya shule. Zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 5000= kila moja.
(i) Jezi nyeusi pair 1 kwa ajili ya michezo.zinaweza kupatikana shuleni kwa tsh. 15,000/=
(j) Track suit **nyeusi** zenye michirizi myeupe zenye nembo ya shule kwa ajili usiku. Zinapatikana shule kwa bei ya Tsh, 30,000/=
(k) Raba nyeupe pair 1 na soksi nyeusi kwa ajili ya michezo na baada ya vipindi vya darasani.
(l) Kandambili nyekundu kwa ajili ya kuogea na viatu vya wazi vya kushindia rangi nyeusi

**NB: Wanafunzi wa kiislamu watatumia hijabu ndefu inayofunika mabega rangi ya nyeupe wakati wa vipindi na hijabu ndefu inayofunika mabega ya rangi ya bluu bahari baada ya vipindi.**

## B: MICHANGO YA SHULE

- Michango ya shule. Tsh. 80,000/= kwa mwaka Fedha za michango ya shule zilipwe kwenye; - Akaunti Na. **31101200105 NMB**
  -Jina la akaunti ni:-***BWIRU GIRLS SECONDARY RECCCURENT ACC***

**MCHANGANUO WA FEDHA KWA AJILI YA MICHANGO MBALIMBALI**

| MCHANGO WA | KIASI | AKAUNTI |
|---|---|---|
| Tahadhari (hazitarudishwa) | 5,000/= | Jina; ***BWIRU GIRLS SECONDARY RECCURENT ACCOUNT*** Acc, No: **31101200105 NMB** |
| Nembo | 5,000/= | |
| Kitambulisho | 5,000/= | |
| GHARAMA YA UENDESHAJI WA SHULE | 65,000/= | |
| Jumla | 80,000/= | |

## B: MALAZI

- **Godoro la futi $2^1/_2$ X 6 (au atakodi shuleni kwa Tsh. 20,000)**
- Blanketi la kujifunika
- Chandarua rangi nyeupe yenye pembe nne.
- Mashuka 2 rangi ya pinki Pamoja na foronya zake.

## C: MATIBABU

**Shule itatoa huduma ya kwanza matibabu kupitia zahanati iliyopo SHULENI Aidha, matibabu makubwa yatagharimiwa na mzazi/mlezi hivyo endapo mwanafunzi ana BIMA aje nayo na asiye na BIMA ya NHIF alipie bima hiyo Tsh. 50,400= kwa mwaka kwenye akaunti ya shule. Na: 31101200105 NMB Jina la akaunti ni:-*BWIRU GIRLS SECONDARY RECCURENT ACCOUNT* ili shule imsaidie kupata BIMA hiyo. Hata hivyo kila mwanafunzi atachangia Tsh. 20,000= kwa mwaka kwa ajili ya huduma ya kwanza matibabu na usafiri Kwenda na kurudi hospitali. Shule haipokei fedha taslimu**. Fedha zote zilipwe kwa kupitia Benki ya NMB, tawi lolote, kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi za malipo (Bank pay-in-slips) zenye jina la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti

## D: MAHITAJI MENGINE

- **Taa ya *kuchaji kwa jua(solar)*** ama Taa ya betri kwa tahadhali ya umeme ukikatika (ISIWE YAKUCHAJI KWA UMEME)
- Kanga/ kitenge jozi moja na Taulo
- Nguo za ndani za kutosha
- Ndoo ya kuogea na dumu la lita 5 jeupe kwa ajili ya maji ya kunywa
- Kandambili jozi moja rangi nyekundu
- Mafuta ya kupaka, Mswaki na dawa ya meno.
- Kijiko, sahani na bakuli(container) na kikombe kwa ajili ya uji Pamoja na tranka kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake

## E: VIFAA VYA USAFI WA SHULE

**Kila mwanafunzi aje na mifagio miwili (02) ya chelewa** ndefu (fagio la wima Iliyofungwa kwa waya na mti )(kila muhula ufagio mmoja) **pamoja na :-**

- Fyekeo 01 – HGE na PMCs
- Reki 01 - PCM.
- Jembe na mpini wake.- PCB
- Hard broom 01 - HGK
- Squeezer (mopper) 01 - CBG
- Ufagio wa buibui( mita4) – HKL
- Soft broom – HGL
- Toilet brush (mpini wa mbao) -EGM

## F: VIFAA VYA MASOMO

- Mabunda mawili (2) ya karatasi A4.*(Ream 2 Double A) kwa mwaka.*
- Madaftari makubwa (Counter books) angalau kumi (10) au zaidi
- Kalamu za wino na za mkaa.
- Vifaa vya masomo kama vile mkebe wa hisabati, calculator,graph pad,dissecting kit& dissecting tray, laboratory coat(nyeupe) kwa wanaosoma masomo ya sayansi na laptop kwa PMCs.
- Kila mwanafunzi aje na vitabu vya masomo yote kulingana na tahasusi yake**.**

## F: MAELEKEZO MENGINE

❖ **MAHUDHURIO**

**Kila mwanafunzi anatakiwa:-**

i) Kuhudhuria shuleni muda wote wa masomo
ii) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
iii) Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
iv) Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba(mabwenini) na madarasani

❖ **MAANDALIO YA JIONI**

**i)** Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie ibada saa 1: 00 – 1:25 na maandalio ya jioni 1:30 - 5:00 usiku na asubuhi saa 11;00-12;30
**ii)** Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila Mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa

❖ **KUWAHI**

Kila mwanafunzi anatakiwa:-

i) Kuthamini muda
ii) Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku
iii) Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa

❖ **SARE ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote:-

i) Masomo darasani
ii) Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
iii) Kwenda hospitali
iv) Baraza la shule
v) Anaposafiri kuja shuleni au Kwenda nyumbani kwao wakati wa likizo
vi) Kazi za mikono (vazi la kazi)
vii) Michezo (vazi la michezo)

**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viatu vyenye visigino virefu, mapambo yoyote pamoja na sare za shule.

❖ **MIPAKA YA SHULE**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

i) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
ii) Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu
  a) Ofisi ya walimu (staff room)
  b) Ofisi zingine za shule
  c) Maabara
  d) Jikoni
  e) Nyumba za walimu / wafanyakazi wasio walimu

- **UGONJWA**
  - i) Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika zahanati ya shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika hospitali.
  - ii) Kila mwanafunzi atachangia Tsh. 20,000= ya huduma ya kwanza matibabu na usafiri hospitali kwa mwaka. Weka kwenye akaunt
  - iii) Mwanafunzi mwenye matatizo lazima amfahamishe matron/ mama malezi wa shule, mara afikapo shuleni
  - iv) Wagonjwa wafike zahanati saa 1: 00 asubuhi kwa ajili ya matibabu kabla ya Kwenda darasani
  - v) Mwanafunzi aje na bima ya afya (NHIF INAYOTUMIKA) au aje na fedha taslimu Tsh 50,400/= kwa ajili ya bima hiyo
- **Nguo za nyumbani haziruhusiwi, mwanafunzi atavaa sare za shule muda wote awapo shuleni na asafiripo kuja shuleni au aendapo nyumbani.**
- Kila mzazi /mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanae kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo na kumpa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi. Ruhusa ya kufuata fedha za matumizi haitolewi. Mzazi unakumbushwa kuwa kumpa mwanao fedha inayopita kiasi, kwaweza kuchangia kuporomoka kwa taaluma yake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Kila mara ahakikishe ni nadhifu kwa nywele fupi zisizozidi urefu wa sentimeta moja na nusu(1.5cm)
- **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu akiwa shuleni. Akija na simu aikabidhi ofisi ya makamu mkuu wa shule hadi rudipo nyumbani atapewa. (HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU SHULENI)**

## G: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**

**7: Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

a) Wizi;
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
f) Kusuka nywele . Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni kwa mtindo uliokubalika na uongozi wa shule;
g) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
h) Uvutaji wa sigara;
i) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
j) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
k) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
l) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
m) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
n) Kudharau Bendera ya Taifa;
o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
p) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Pia Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo**:-

(i) Kukata sare ya shule
**(ii)** Kwa yule atakayependa kushonea shuleni, HATARUHUSIWA kuja shule na nguo za nyumbani **(Ataruhusiwa kuja na sare ya shule atokayo**

**pamoja na track – suit 1 wakati akisubiria kupewa sare za shule yetu.)**

(iii) Kunyoa mitindo ( Panki, kiduku n.k)

(iv) Ni mwiko kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi bwenini. Ukiwa nayo, kabidhi kwa Mwalimu wa malezi na utatumia kwa maelekezo

(v) Ni mwiko kumiliki simu, vidani, vipodozi na perfume.

(vi) Ni mwiko kuja na vyakula shuleni na kupeleka vyakula bwenini.

(vii) Ni mwiko kutoka nje ya shule bila kibali. Endapo umeruhusiwa, tembea na kibali chako na urudi shuleni kwa wakati ulioelekezwa.

**NB: MUDA WA KUINGIA SHULE MWISHO NI SAA 9:30 JIONI. TAFADHALI ZINGATIA MUDA**

## 8: VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu zibandikwe kwenye fomu.
v. Picha 2 za mwanafunzi
vi. Ulete kivuli cha cheti cha kuzaliwa .

NB:- TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU TAFADHALI FOMU HIZI ZILETWE SIKU YA KURIPOTI SHULENI.

- Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI MZAZI/MLEZI, UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA**

## KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

*Moto wa Shule*: **ELIMU NA KAZI**

HEADMISTRESS
BWIRU GIRLS HIGH SCHOOL
P. O. Box 170, MWANZA

**CHRISTINE E. ZEGERA**
**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**
**SHULE YA SEKONDARI BWIRU GIRLS'**

## FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

1 .Jina kamili la mzazi/mlezi..........................................................................
2. Mahali anapoishi kwa sasa..........................................................................
3. Anwani ya mzazi/mlezi huyo ni --------------------------------------------
4 .Namba yake ya simu ni .............................................................. 5 .Kabila lake……......
6. Dhehebu/Dini..................................................................................
7.Jina la mwenyekiti wa kitongoji..........................................sahihi na Muhuri................
Mimi [ mzazi/mlezi atakayeandikishwa shuleni ]......................................ambaye ni mzazi/mlezi wa............................................................................ [Jina la mwanafunzi] wa kidato...... ...mwaka..............
Nakiri kuwa nitakubaliana na kufuata sheria, kanuni na maelekezo mengine ya shule kadri yatakavyotolewa na uongozi wa shule.

**NITALIPA MICHANGO YOTE YA SHULE BILA USUMBUFU WOWOTE KWA SHULE WALA KWA MWANAFUNZI ILI KUMUWEZESHA MWANAFUNZI ASOME VIZURI.**

**NITAFUATILIA MAENDELEO YA MWANAFUNZI KILA MWEZI NA KUSHIRIKI VIKAO VYA KITAALUMA ILI KUHAKIKISHA MTOTO ANAKAMILISHA MALENGO YAKE ILI KUHAKIKISHA MWANANGU ANAFAULU ZAIDI YA WASTANI WA SHULE AMBAO NI 61%**

................................................ ...............................
mzazi/mlezi Tarehe

## AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE, KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi [ mwanafunzi] ……………………………. Wa kidato …… mwaka ……… naahadi kufuata sheria na taratibu zote za shule kadri zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule muda wote niwapo shuleni na kwamba sitashiriki migomo, fujo wala makosa yoyote ya jinai. Pia naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwa uongozi wa shule na jumuiya nzima ya BWIRU GIRLS Sekondari. Nitajifunza kwa bidi na weledi ili kufikia ufaulu wa zaidi ya wastani wa shule ambao ni 61%.

............................................ ...................
Saini ya mwanafunzi Tarehe

............................ ............................. ..........
Jina la mzazi/mlezi saini ya mzazi/mlezi tarehe

**SHULE YA SEKONDARI BWIRU GIRLS'**
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

**1.** Jina kamili (Kama ilivyo kwenye *PREM/PREM*) ......................................
**2.** Anwani ya nyumbani S.L.P ………….……………….. WILAYA ..............................
**3.** Tarehe ya kuzaliwa .........…………...……………………………………………………
**4.** Mahali ulipozaliwa, Kijiji …………………........…… Kata ……................… Tarafa ……….
**5.** Mahali unapoishi kwa sasa ……………………….............…………. WILAYA …………..…
**6.** Shule ya sekondari ulikotoka……………………..……Anwani…………………………………
**7.** Dini/Dhehebu ……………………………..........………Kabila………………………………
**8.** Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa muhimu kwa masuala yahusuyo shule:

**(i)** Jina la Baba …………………………………………… Namba ya simu ……......................
Hai/Si hai ...............(kama hai) kazi yake ................…......... Anwani .................

**(ii)** Jina la mama ………………………………………..Namba ya simu ……..................................
Hai/Si hai........................ (kama hai) kazi yake ...............…......... Anwani …………....…

**(iii)** Jina la Mlezi ………………………………. Uhusiano …………………… Namba ya simu ……….…
kazi yake ……….…..... Anwani S.L.P……………….. WILAYA ………..

**(iv)** Jina la Mlezi …………………………..Uhusiano………………Namba ya simu………
kazi yake ……….........………. Anwani S.L.P……………….. WILAYA ……………

**NB: BANDIKA PICHA ZA WANAOHUSIKA HAPO JUU KWENYE VIBOMA**

| PASIPOTI BABA | PASIPOTI MAMA | PASIPOTI MLEZI | PASIPOTI MLEZI |
|---|---|---|---|
| SIMU ……….................... | ................................ | .......................... | ........................ |

Mimi (Mwanafunzi) ………………………………………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

...................................................... ..........................
**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)
……………………………………………………………………………………………………….
ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………....nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari BWIRU GIRLS' ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

........................................................ ………………
**Saini ya Mzazi/Mlezi** **Tarehe**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCALGOVERNMENT**

**ILEMELA MUNICIPAL COUNCIL**

**BWIRU GIRLS' SECONDARY SCHOOL**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**(TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER IN A HEALTHY CENTRE OR DISTRICT HOSPITAL)**

**Student's full name……………………………………………………………….……...............**

**Age…………………………. years ………………...** **sex………………………………..............**

**Stool examination………………………………………………………………...........…**

**Urinalysis……………………………………………………………..………..............…...**

**Blood count (red &white) ………………………………………………..……..…..........................**

**Syphilis test………………………………………………………………......….......................................................**

**Spleen……………………………………………………………………..........................................**

**Mental condition………………………………………………………...………….................................................**

**Sight…………………………………………………………………………..………………...........**

**Chest (T.B) ………………………………………………………………………………...................................................**

**Pregnancy ....………………………………………………………………………………...................................................**

**ADDITIONAL INFORMATION (e.g. physical defects, impairments or chronic disease requiring special treatment/attention)**

**.............................................................................................................................................**

**.............................................................................................................................................**

**.............................................................................................................................................**

**...........................................................................................................................................**

**I certify that I have examined the above student and recommend that he/she is fit/unfit to pursue his/her secondary education studies**

**Signature…………………………………………….**

**Designation………………………………………….**

**Official stamp……………………………………….**

**Date………..**

**ORODHA YA VITABU VYA A- LEVEL**

**PHYSICS**

1. PHYSICS FOR SEC SCHOOLS FORM FIVE AND FORM SIX (TIE S.
2. CHAND'S PRINCIPLE OF PHYSICS FOR CLASS XI AND XII
3. ROGER MUNCHASTER
4. NELKON AND PARK. PRINCIPLE OF PHYSICS
5. TOM DUNCAN

**BIOLOGY A – LEVEL**

Dr. Charles M. Lyimo. (2019). Biology for Advance Level Secondary School Student Book Form Five. Dar es salaam; Tanzania institute of education.

Campbell R, Urry C.W and Minorsky J. (2008). *Biology (Eight Edition).* San Francisco CA 94111: Pearson Benjamin Cumming,1301 Sansome St.Connie R, Robert W, Vladimir J, Jean D, Jung C, Yael A. (2017). *Biology.* Rice university: Openstax.

Dr. Dr Neema G. Mogha, et el, (2019). Biology for Advance Level Secondary School Student Book Form Six. Dar es salaam; Tanzania institute of education.

Glenn Toole and Susan Toole, (1987). Understanding Biology For Advance Level (4th ed). ISBN9780748739578.

L.K, M. (1992). *Biology series.* Dar es salaam: Mture Publishers.

Raven, J. *Biology (six edition).*

Taylor D.J, Green N.P.O, Stout GW. (2002). *Biological science (Third edition).* Cambridge University Press: P.t Ltd Kundli 131028.

Verma P.S and Pandey B.P. (2005). *S. Chands Biology for class XII.* New dehl: S. Chand and Company Ltd, Ram Nagar.

Verma P.S, Pandey B.P, Chand's S. (2002). *Biology for class XI.* New Delhi: Chand S and Company Ltd. Ram Nagar.

**CHEMISTRY A – LEVEL**

1. CHEMISTRY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE (TIE)
2. PRINCIPLES OF CHEMISTRY – BY CHAND CLASS XI, AND XII
3. MODERN ABC{PART 1 AMD 2} BY DR.SP JAUHAR
4. MZUMBE BOOK PROJECT

**KISWAHILI**

1. FASIHI KWA UJUMLA
2. TAHAKIKI
3. KISWAHILI KWA SHULE ZA SEKONDARI(KIDATO CHA TANO NA SITA) - TIE

**VITABU TEULE**

A: RIWAYA

a) Dunia uwanja wa fujo
b) Ua la faraja
c) Mirathi ya hatari
d) Wasifu wa Siti Binti Saad

B;TAMTHILIYA

- **Mkwaya wa uhehe**
- **Shujaa mirambo**
- **Usaliti mjini**

C; USHAIRI

- **Fumbo linaloelea**
- **Malenga wa ziwa kuu**
- **Andamo: msafiri safarini**
- **Wosia wa baba**

**ENGLISH LANGUAGE**

1. ENGLISH FOR ADVANCED LEVEL ( FORM FIVE AND SIX) BY TIE
2. (ASHELI, N (20100 2ND EDITION. ADVANCED LEVEL ENGLISH: A PRACTICAL APPROACH
3. OXFORD ENGLISH DICTIONARY

**PLAYS:**

- The government inspector
- An enemy of the people
- A taste of heaven

4. **NOVELS AND SHORT STORIES**
    - A. Animal farm
    - B. Chasing the leopard finding the lion
    - C. The opportunist elite
    - D. The horizon unveiled
5. **POEM**
    - Summon; poem from Tanzania
    - Poets of Africa; lament of the silent and other poems

**GEOGRAPHY**

- A. MAP SHEET BOOK
- B. MSABILA, D.T (2003). A COMPREHENSIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOL
- C. MSABILA, D.T (2008) . AN INTEGRATED REGIONAL STUDY ON HUMAN NJIKU, J.W & SALASU, J.F.K (2008) THE ESSENTIALS OF PRACTICALS GEOGRAPHY ADVANCED LEVEL FORM 5 & 6.
- D. TRURAN, H.C . A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAP AND DIAGRAMS.
- E. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCE SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE AND SIX (TIE). PRACTICAL, PHYSICAL HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY (TIE)
- F. KAMIL, Z. PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVES
- G. GENERAL GEOGRAPHY IN DIAGRAM – RB BUNNETT

**HISTORY**

- A. TIE(2024) HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS. STUDENT'S BOOK FORM V
- B. NDARO, S.A(2023) AFRICAN HISTORY FOR ADVANCED LEVEL. HISTORY PAPER
- C. MANDAYA, B.(2025) HISTORY FOR ADVANCED LEVEL FORM FIVE
- D. MANDAYA, B.(2025) HISTORY FOR ADVANCED LEVEL FORM SIX

**HISTORIA NA MAADILI YA TANZANIA**

- A. TIE(2021) HISTORIA NA MAADILI YA TANZANIA

**ACADEMIC COMMUNICATION**

**A: TIE(2021)** ACADEMIC COMMUNICATION

**ADVANCED MATHEMATICS**

- A. PURE MATHEMATICS 1 ( L. BOSTOCK, S CHANDLER
- B. S.CHAND'S MATHEMATICS FOR CLASS XI (H.K DASS & DR. RAMA VERMA)
- C. (TIE) ADVANCED MATHS FORM V & VI
- D. CONCISE ADVANCED MATHS By Mayombya
- E. ADVANCED MATHEMATICS BY Tranter

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

- **(TIE) BASIC APPLIED MATHS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENTS' BOOK FORM V&VI**

**ECONOMICS**

1. ***MICROECONOMICS – FIVE – TIE***
2. ***MACROECONOMICS – SIX – TIE***
3. ***ECONOMICS I BY AMBROS ODHIAMBO***
4. ***ECONOMICS II BY AMBROS ODHIAMBO***

**COMPUTER**

***. COMPUTER SCIENCE FOR ADVANCED FORM FIVE (TIE)***

***. COMPUTER SCIENCE for advanced level form six (TIE)***

***. COMPUTER ALLOGARITHS FOR ADVANVED LEVEL***